© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Asili: Kanda ya tepu ijulikanayo kwa jina la **Haadhihi Da'watunaa** (Hii ndiyo Da'wah yetu), asili yake ikiwa ni kwa lugha ya Kiarabu ilitolewa na *Shoor Lil-Intaaj Al-Islaamee*, na baadae ikanukuliwa na kufasiriwa kwa lugha ya kizungu na al-manhaj.com. Nakala hii ni tafsiri ya kanda asili iliyofanyiwa marekebisho kwa min-ajil ya usomaji bora.

Ibraaheem: Kwa jina la Allaah, kila Sifa njema ni za Allaah, Amani na Baraka za Allaah zimshukie Mtume Wake (Sallallaahu 'alayhi wasallam).
Kwanza kabisa: Kwa hakika Allaah (Subhaanahu wata'aalah) Ametuteremshia Baraka za Eemaan, na vilevile Akaubariki Ummah mzima wa Ki-Islaam kwa Wanavyuoni - ambao ndiwo waliotukuzwa na Allaah kwa kupewa Ilimu - ili (kwa ilimu hiyo) wapate kuwaongoza watu juu ya njia ya Allaah na juu ya njia ya Ibaadah ya Allaah ("Azza wa-jallah). Hapana shaka yoyote yakwamba wao ndiwo warathi wa Mitume. Sababu ya kujumuika hapa sisi, Insha Allaah, kwanza kabisa ni kumridhisha Allaah na pili ni kutafuta ilimu, ambayo matokeo yake ndiyo yatakayo-tuelekeza kwenye Radhi za Allaah. Kwani, Wallaahi, huu ni wakati wa furaha - kwa vile tumeweza kujumuika pamoja na Sheikh wetu na Mwanachuoni wetu, na mwalimu wetu mkuu, Sheikh Muhammad Naasir-ud-Deen Al-Albaanee. Mwanzo kabisa, kwa niaba ya mkusanyiko huu tungelipenda kumkaribisha muheshimiwa Sheikh wetu, na hal-kadhaalika kwa niaba ya kila anaesikiliza, haswa wale wanafunzi wa ki-elimu, wote hao pia wanamkaribisha nao wanatamani kujumuika pamoja na muheshimiwa mwalimu wetu. Na bila ya shaka, sote sisi tunayo matamaniwa kama hayo ya kuisikiya ilimu na hikma aliyonayo. Kwahivyo, hebu tumsikilizeni kwa yale ambayo Allaah Aliyombariki nayo katika ilimu. Kisha baadae, Sheikh wetu atakapoamua kufunga muhaadhara huu, ukumbi wa masuali utafunguliwa, lakini itabidi masuali yenyewe yaandikwe kwenye karatasi ambazo tutakazo wagawanyia - Insha Allaah. Tunarudia tena kusema, "Huu ni wakati wa furaha na tunasema, Ahlan, karibu, kwa muheshimiwa Sheikh wetu...

Sheikh: Ahlan Bikum. Kila Sifa njema ni zenye kumthubutukia Allaah, Tunamsifu Yeye,

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

na tunatarajia msaada Wake na msamaha kutoka Kwake. Tunajilinda kwa Allaah (Subhaanahu wata'aalah) kutokana na maovu ya nafsi zetu na kutokana na udhaifu wa vitendo vyetu. Yeyote alieongozwa na Allaah, hakuna yeyote awezae kumpotoa, na Yeyote aliepotolewa na Allaah, hakuna yeyote awezae kumuongoza. Nashuhudia yakwamba hapana mungu wa kweli anaestahiki kuabudiwa isipokuwa Allaah, Peke Yake, pasi na mwenzi wala mshirika. Nazidi kushuhudia yakwamba Muhammad ni Mtumwa wake wa kweli na Mtume. Ammaa Ba'ad: Kwa hakika maneno yalio ya kweli kabisa ni yale ya Kitabu cha Allaah (Qur'aan) na uongofu ulio bora zaidi ni ule wa Muhammad (Sallallahu 'alayhi wasallam). Na maovu yalio mabaya zaidi ni mambo ya kuzua (yalio mageni katika mafundisho ya Uislamu), na kila jambo lilozuliwa (katika Dini) ni Bid'ah, na kila Bid'ah ni Dhalaalah (njia mbaya, upotofu), na kila Dhalaalah mwisho wake ni motoni.

Namshukuru ndugu, ustaadh Ibraaheem kwa maneno yake na kwa kusifu kwake... Na mimi sina la kusema katika kuyajibu hayo isipokuwa kufuata mfano wa Khaleefah wa kwanza, Abu Bakr As-Siddeeq (Radhiallaahu 'anhu), ambae ndie aliyekuwa Kaleefah wa kwanza wa Rasoolullaahi (Sallallaahu 'alayhi wasallam) aliyestahiki. Walaakin alipokuwa akimsikiya mtu akimsifu kwa mambo ya kheri na akiamini yakwamba sifa hizo, bila ya kujali zinasifiwa na nani, zimetiwa chumvi (maongezo) - na hayo yalikuwa katika wakati wa ukhalifa wake, ambapo alistahiki kusifiwa kwazo - lakini... - [Mara vilio vikaanza kusikika] - lakini alikuwa akisema:

"Yaa Allaah, Usinipatilize kutokamana na wayasemayo (kunihusu mimi). Na unija'alie niwe bora kuliko wanavyoniona (mimi nilivyo). Na Unisamehe kwa yale wasoyajua (kunihusu mimi)."

Haya ndiyo Bwana As-Siddeeq aliyokuwa akiyasema. Sasa jee kutuhusu sisi tulokuja baada yake tusemeje? Mimi nasema, fuata mfano wake: "Yaa Allaah, Usinipatilize kutokamana na wayasemayo (kunihusu mimi). Na unija'alie niwe bora kuliko wanavyoniona (mimi nilivyo). Na Unisamehe kwa yale wasoyajua (kunihusu mimi)."

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Nitajaliza katika hayo kwa kusema yakwamba mimi siye huyo mtu aliye-elezwa katika yale mliyokwisha kuyasikiya hivi punde kutoka kwa ndugu yetu mheshimiwa Ibraaheem. Bali mimi ni mwanafunzi tu ninaetafuta ilimu; na wala si chengine chochote. Na ni juu ya kila mwanafunzi ashikamane na hadeeth ya Rasoolullaahi (Sallallaahu 'alayhi wasallam) isemayo: **"Fikilizeni kutoka kwangu hata kama ni Aayah moja. Na simulieni kutoka kwenye (hekaya za) kizazi cha Israa'eel, kwani hapana madhara. Na yeyote anizuliae mimi urongo kwa kukusudia, basi na ajiandalie makaazi yake motoni."**

Kwahivyo, kwa kujiegemeza juu ya hadeeth hii na kujisalimisha na matamshi haya matukufu ya ki-Utume, pamoja na matamshi mengine yatokayo kwenye kitabu cha Allaah na hadeeth za Rasoolullaahi (Sallallaahu 'alayhi wasallam), tunajitweka jukumu la kuwatangazia watu yale yaliyowapungukia katika ilimu. Wala hii haina maana yakwamba sisi ndio tumekuwa kama yale yanayopatikana katika fikra njema ambazo (baadhi ya) ndugu zetu wanazotufikiria nazo. Mambo hayendi hivyo. Huu ndiwo ukweli ulio ndani ya moyo wangu. Kila nisikiapo maneno ya aina hii, hukumbuka methali moja ya zamani, ijulikanayo sana miongoni mwa wanavyuoni:

"Kwa hakika, kidege *(bughaath)* kwenye miji yetu amekuwa Tai."

Baadhi ya watu hawatambui yaliyokusudiwa kwa maneno haya au kwa methali hii. Bughaath ni kijidege kisichokuwa na thamani yoyote - lakini kijidege hichi huwa kama Tai kwa watu - kutokana na ujinga wao...

Methali hii ni ya kweli kuwahusu watu wengi wanaolingania watu kwenye Uislamu, iwapo wako juu ya haki na uongofu au juu ya makosa na upotofu. Lakini Allaah Anajua yakwamba Ulimwengu mzima wa Ki-Islamu ni patupu - isipokuwa kwa watu wachache mno ambao, ni sawa kusema kuwahusu wao yakuwa "Fulani ni mwanachuoni." Kama ilivyosemwa katika hadeeth Saheeh, iliyopokewa na Imaam al-Bukhaaree kwenye Saheeh yake, kutoka katika riwaya ya 'Abdullaah Ibn 'Amr Ibn al-'Aas (Radhiallaahu 'anhu) aliyesema: Amesema Rasoolullaah (Sallallaahu 'alayhi wasallam):

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

"Kwa hakika, Allaah Hatoinyakuwa ilimu kutoka kwenye vifua vya wanavyuoni, lakini Ataichukuwa Mwenyewe ilimu kwa kuwaondoa wanavyuoni. Mpaka pasibakie mwanachuoni yoyote - hii ndiyo nukta yenyewe - **mpaka pasibakie mwanachuoni yoyote, watu watachukuwa viongozi wajinga watakaoulizwa maswali na kisha watoe fatwaa (hukmu za ki-Dini) bila ya ilimu. Basi wao watapotea na kuwasababisha wengine kupotea."**

Allaah Anapotaka kuichukuwa ilimu, hatoinyakuwa kutoka vifuani mwa wanavyuoni, ikawa wanavyuoni ni kama watu ambao hawajawahi kusoma chochote mwanzoni, Laa! Hii si katika Sunnah (njia) ya Allaah Anavyofanya kuhusu mja wake, haswa waja wake wema - kuinyakuwa ilimu ambayo waliyojipatia kwa ajili ya Allaah "Azz wa Jall... Allaah ni Muadilifu na Mwenye kufanya haki katika hukmu zake - Hainyakuwi ilimu kutoka katika nyoyo za wanavyuoni wa kikweli. Lakini ni miongoni mwa Sunnah za Allaah pindi Anapoichukuwa ilimu kutoka kwa viumbe vyake, huiondoa kwa kuwachukuwa wanavyuoni wake [yaani: Kuwafisha - kuwaondolea Uhai] kama Alivyofanya kwa kiongozi wa wanavyuoni na Mitume wote, Muhammad (Sallallaahu 'alayhi wasallam).

"...Mpaka pasibakie mwanachuoni yoyote, watu watachukuwa viongozi wajinga watakaoulizwa maswali na kisha watoe fatwaa (hukmu za ki-Dini) bila ya ilimu. Basi wao watapotea na kuwasababisha wengine kupotea."

Hii haimaanishi yakwamba Allaah Atauwacha Ulimwengu bila ya kuwepo mwanachuoni, ambae kwa kupitia kwake ndipo unapoweza kuthibitishwa ushahidi juu ya watumwa wake, lakini maana yake ni kwamba, kila unapozidi kupita wakati, ilimu nayo inazidi kupungua. Na tutaendelea kuzidi katika hali hii ya kuwa na ilimu chache na pungufu, mpaka pasibaki juu ya uso wa ulimwengu huu, yeyote asemae: **"Allaah, Allaah."** Mushaisikiya hadeeth hii mara nyingi, ambayo ni hadeeth saheeh:

"Kiyama hakitosimama kukawa kumebaki mtu juu ya uso wa ulimwengu, asemae: 'Allaah, Allaah.'"

Miongoni mwa mfano wa watu hao waliotajwa katika sehemu ya mwisho ya hadeeth hiyo: **"mpaka pasibakie mwanachuoni yoyote, watu watachukuwa viongozi wajinga"** ni wale viongozi wanaofasiri Qur'aan na Sunnah kwa kuzitumia tafsiri zenye kwenda kinyume na misimamo ya wanavyuoni - sitosema wale wa zamani peke yao, lakini vilevile wale walio hai katika zama zetu. Kwani kwa hakika wanaitumia hadeeth hii **"Allaah, Allaah"** kama ndio ushahidi wao wa kuruhusiwa, bali mapendekezo ya kumkumbuka Allaah (kwa kufanya dhikiri) kwa kutumia neno moja moja - Allaah, Allaah, Allaah, na kadhaalika, kama inavyofanywa na ma-Soofee. Ili mtu yoyote asidanganyike au akawa hajajitayarisha anaposikia hadeeth hii na hiyo tafsiri yake ya upotofu, nafikiri ni jambo la sawa, hata kama hatukulipangilia, kuwakumbusha ndugu zetu hapa yakwamba tafsiri hii ni baatil (ya upotofu), kwanza kwasababu ufafanuzi wa hadeeth hiyo umebainishwa katika riwaya nyengine ya Rasoolullaah (Sallallaahu 'alayhi wasallam). Na pili, lau kama tafsiri hii ingelikuwa ni ya sawa, pangelikuwa na ishara yake katika vitendo vya watangulizi wetu wema (Salaf As-Saalih), Allaah Awe radhi nao. Kwahivyo, iwapo wao hawakulifanya jambo hilo - Basi huko kukataa kwao kuifuata tafsiri hiyo inaonyesha ishara ya urongo wa tafsiri kama hiyo. Sasa utakuwaje utakapo-onyeshwa hiyo riwaya nyengine, na maana yake, kama inavyosemwa kwa kawaida, ni kwamba Imaam Ahmad (Rahimahullaah) akaipokea hadeeth hii katika Musnad yake kwa upokezi ulio saheeh, kwa maneno yafuatayo:

"Kiyama hakitothibitishwa na ikawa atabakia mtu juu ya uso wa ulimwengu asemae: 'Laa Ilaaha Illaa Allaah'"

Haya ndiyo yaliyo kusudiwa katika hadeeth ya kwanza, pale ambapo neno **"Allaah"** limekaririwa. Jambo lililoko hapa ni kwamba leo, kwa bahati mbaya ulimwengu mzima umewapa nyongo wanavyuoni hao waliokuwa wakiujaza ulimwengu mzima kwa ilimu zao kunjufu na kuweza kuwafikilizia watu. Leo imekuwa kama ulivyo msemo usemao:

Walipohisabiwa walionekana kuwa ni wachache mno
Lakini leo wamepungua kuliko ile idadi ya uchache wao.

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Kwahivyo tunatarajia kutoka kwa Allaah ('Azza wa-Jallah), Atuja'alie tuwe ni miongoni mwa wenye kutafuta ilimu, (wale) ambao wanaoiga kihakika kutoka katika mifano ya wanavyuoni na wanaofuata njia yao kwa uaminifu. Haya ndiyo matarajio yetu kutoka kwa Allaah ('Azza wa-Jallah) - Atuja'alie tuwe ni miongoni mwa wale wanafunzi wenye kufuata njia hiyo ambayo Rasoolullaah (Sallallaahu 'alayhi wasallam) aliyosema:

"Yeyote mwenye kufuata njia kwa ajili ya kutafuta ilimu, Allaah Atamtengezea njia ya kuelekea peponi."

Jambi hili litatuongoza katika kulizungumzia suala la ilimu hii, iliyotajwa ndani ya Qur'aan, mahali kwingi sana , kwa mfano maneno Yake Allaah (Subhaanahu wata'aalah) (kama yalivyofasiriwa):

قُلْ هَلْ يَسْتَوِي ٱلَّذِينَ يَعْلَمُونَ وَٱلَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ

"Sema: 'Je, wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua?'" [Soorah az-Zumar 39:9]

Akasema tena ('Azza wa-Jallah) (kama yalivyofasiriwa):

يَرْفَعِ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مِنكُمْ وَٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْعِلْمَ دَرَجَٰتٍ

"Allaah Atawainua wale walioamini miongoni mwenu; na waliopewa ilimu watapata daraja zaidi." [Soorah al-Mujadilah 58:11]

Ni ilimu gani hii ambayo kwayo, Allaah ('Azza wa-Jallah) Aliwasifu wenye nayo na wakaihudumikia pamoja na wale wenye kuifuata njia ya watu hao? Jawabu ni kama alivyosema Imaam Ibn al-Qayyim Al-Jawziyyah (Rahimahullaah), mwanafunzi wa Sheikh ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahullaah):

"Ilimu ni: (yale) Aliyoyasema Allaah, (yale) aliyoyasema Mtume Wake, (na yale) waliyoyasema Maswahaba zake. Hili si jambo la urongo.

Ilimu si kujivurumiza katika kukhilafiana bila ya kuwa na mazingatio kati ya Mtume na kati ya rai ya faqeeh (mwanachuoni).

Sivyo hivyo, na wala sisi hatukanushi na kuzipinga Sifa za Allaah, kwa kukhofia tu tusije tukatumbukia ndani ya tashbeeh na tamtheel."

Kwahivyo tunachukuwa ufafanuzi wa ilimu kutoka katika maneno haya na mashairi haya, ambayo ni nadra kuyasikia miongoni mwa mitungo ya mashairi, kwani mashairi ya wanavyuoni si kama mashairi ya washairi. Mtu huyu (Ibn al-Qayyim) alikuwa ni mwanachuoni, na vile vile aliwahi kuandika mashairi mazuri. Akasema: Katika daraja ya kwanza, Ilimu ni: (yale) Aliyoyasema Allaah, kisha (ni yale) aliyoyasema Rasoolullaah (Sallallaahu 'alayhi wasallam), katika daraja ya pili, kisha (ni yale) waliyoyasema Maswahaba, katika daraja ya tatu.. Maneno ya Ibn al-Qayyim yanatukumbusha kuhusu ukweli ulio na umuhimu mkubwa, na ambao mara nyingi hupuuzwa na kikundi kikubwa cha walinganizi waliotapakaa kila mahali ulimwenguni kwa jina la Uislamu. Ukweli huo ni upi? Kinachofahamika vizuri kwa walinganizi wote hawa ni kwamba asili ya Uislamu ni: Kitabu cha Allaah na Sunnah za Rasoolullaah (Sallallaahu 'alayhi wasallam). Huu ni ukweli usio na shaka, lakini una upungufu ndani yake. Na upungufu huu umeandikwa na Ibn al-Qayyim katika mistari yake ya mashairi ambayo tuliyokwisha kuyataja. Hiyo ndiyo sababu baada ya kuitaja Qur'aan na Sunnah, aliwataja Maswahaba. "Ilimu ni: (yale) Aliyoyasema Allaah, (yale) aliyoyasema Mtume Wake, (na yale) waliyoyasema Maswahaba zake..."

Siku hizi ni nadra sana kumsikia mtu akiwataja Maswahaba anapozitaja Qur'aan na Sunnah. Na kama tujuavyo sote sisi, yakwamba wao ndiwo walio katika kichwa cha Salaf As-Saalih (wema waliotutangulia), ambao Rasoolullaah (Sallallaahu 'alayhi wasallam) aliwazungumzia aliposema, na kupokelewa na maswahaba wengi:

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

"Bora ya watu ni (wa) qarne yangu..."

Na usiseme kama wasemavyo wengi wa wanaojishughulisha na ulinganizi: **"Bora ya qarne."** Maneno haya, **"bora ya qarne."** hayana asili yoyote katika Sunnah. Sunnah iliyo saheeh, ambayo iliyonukuliwa kwenye saheeh mbili (Bukhaaree na Muslim) na kumbukumbu ya Ahaadeeth nyengine, zote zimeitaja hadeeth hiyo kwa maneno: **"Bora ya watu ni (wa) qarne yangu, kisha ni wale waliokuja baada yao, kisha ni wale waliokuja baada yao."**

Imaam Ibn al-Qayyim Al-Jawziyyah amewaunganisha Maswahaba hawa - ambao ndio walioko katika kilele cha qarne hizo tatu na wakapokea ushuhuda wa ubora - na kitabu na Sunnah. Sasa huku kuunganisha kwake kulikuwa ni rai yake, au ni makisio ya Uwana-chuoni na uamuzi wake, ambayo yote yanaelekea kwenye makosa. Jawabu ni la! hayo hayatokani na makisio ya Uwana-chuoni wake au uamuzi wake, ambao una uwezekano wa kuingiana na makosa, bali imeegemezwa juu ya kitabu cha Allaah na hadeeth za Rasoolullaah (Sallallaahu 'alayhi wasallam). Amma kwa Qur'aan, kuna maneno Yake Allaah (Subhaanahu wata'aalah) (kama yalivyofasiriwa):

وَمَن يُشَاقِقِ ٱلرَّسُولَ مِنۢ بَعۡدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ ٱلۡهُدَىٰ وَيَتَّبِعۡ غَيۡرَ سَبِيلِ ٱلۡمُؤۡمِنِينَ نُوَلِّهِۦ مَا تَوَلَّىٰ وَنُصۡلِهِۦ جَهَنَّمَۖ وَسَآءَتۡ مَصِيرًا ﴿١١٥﴾

"Na atakayemwasi Mtume baada ya kumdhihirikia uwongofu na akafuata njia isiyokuwa ya Waumini, tutamgeuza alikogeukia mwenyewe na tutamwingiza katika jahannam; napo ni pahali pabaya kabisa pa mtu kurudia." [Soorah an-Nisaa' 4:115]

"Na akafuata njia isiyokuwa ya Waumini" - Mola wetu Hakuikatiza Aya hii, kama Angelifanya hivyo, vilevile Aya hiyo ingelikuwa ni sawa na ya kweli. Hakusema: **"Na**

atakayemwasi Mtume baada ya kumdhihirikia uwongofu, tutamgeuza alikogeukia mwenyewe na tutamwingiza katika jahannam; napo ni pahali pabaya kabisa pa mtu kurudia."

Badala yake, kutokana na hikma zake zisokifani, Aliongezea **"Na akafuata njia isiyokuwa ya Waumini"** - na hili ndilo tulilokusudia kulizungumzia sasa.

"Na atakayemwasi Mtume baada ya kumdhihirikia uwongofu na akafuata njia isiyokuwa ya Waumini, tutamgeuza alikogeukia mwenyewe na tutamwingiza katika jahannam; napo ni pahali pabaya kabisa pa mtu kurudia." [Soorah an-Nisaa' 4:115]

Natumai Aya hii itakita katika fahamu zenu na nyoyo zenu, na natumai pia yakwamba hamutoisahau, kwa sababu huwo ndiwo ukweli. Na kwa ukweli huwo, mutanusuriwa na upotofu ulioko upande wa kulia na upande wa kushoto, na munusuriwe - hata kwenye mas-ala fulani au jambo kadhaa - musije mukatumbukia ndani ya mojawapo ya mapote ambayo hayatonusuriwa; au mojawapo ya mapote ya upotofu. Hii ni kwa sababu Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam) alisema katika hadeeth mashuhuri sana, ambayo nitakayo ifupisha ili tuipate ile sehemu inayolingana na mazungumzo yetu:

"Na Ummah wangu utagawanyika katika makundi sabiini na tatu - yote hayo yatakuwa ni ya motoni, isipokuwa moja". Wakasema: **"Ni lipi hilo, Yaa Rasoolullaah?"** Akasema: **"(Kundi hilo) ni Jamaa'ah."**

Jamaa'ah ni **"Njia ya waumini."** Kwahivyo hiyo hadeeth - ikiwa si wahyi wa moja kwa moja kutoka kwa Allaah hadi katika moyo wa Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam), basi hapana budi yakwamba imechukuliwa kutoka katika Aya tuliyotangulia kuitaja. **"Na akafuata njia isiyokuwa ya Waumini"** Kwahivyo kwa yule mwenye **"Kumpinga Mtume"** na **"akafuata njia isiyokuwa ya Waumini"** amehofishwa na moto wa Jahannam, kisha kinyume chao pia ni sawa, na anaeandama **"Njia ya waumini"** - basi ata-ahidiwa Pepo, na hilo ni jambo lisilo na shaka. Kisha-basi, Rasoolullaahi (Sallallaahu 'alayhi wasallam) alilijibu suala lililohusu pote litakalo nusuriwa, akasema: ***"Jamaa'ah*** .

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Basi jamaa'ah ni kundi la Waislamu. Halafu kukatajwa kwenye riwaya nyengine ya hadeeth hii, jambo linalounga mkono muelekeo huu, kwa kweli imeongeza ubainifu na ufafanuzi wake. Akasema Rasoolullaahi (Sallallaahu 'alayhi wasallam):

"Ni yale ambayo mimi na maswahaba zangu tuliyojiegemeza kwayo."

"Maswahaba zangu", kwahivyo ndiyo **"Njia ya waumini"**. Imaam Ibn al-Qayyim alipowataja maswahaba katika mistari yake ya mashairi tuliyoyataja, aliyachukuwa mafunzo hayo kutoka katika Aya tulokwisha kuitaja na hadeeth hii. Vile-vile ipo hadeeth nyengine mashuhuri sana ya Al-'Irbaad ibn Saariyah (Radhiallaahu 'anhu), ambayo pia nitaifupisha kwa kutaja sehemu inayolingana na mazungumzo yetu, ili tuwe na nafasi ya kutosha ya kupokea masuali yenu. Akasema Rasoolullaahi (Sallallaahu 'alayhi wasallam):

"Basi shikamaneni na Sunnah zangu na Sunnah za Makhalifa walio juu ya uongofu (watakaokuja) baada yangu."

Sasa hapa tunaona mfano uleule kama hadeeth tuliyokwisha kuitaja kabla ya hadeeth hii na vile-vile Aya iliyotangulia. Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam) hakusema "Shikamaneni na Sunnah zangu" peke yake, lakini badala yake alizifungamanisha Sunnah zake na Sunnah za Makhalifa (wake) walio juu ya uongofu. Mpaka kufikia kiwango hichi, tunasema, haswa kwenye zama zetu hizi zilizojaa mawazo ya upinzani, mifumo, madhaahib, idadi kubwa ya vikundi na vipote, mpaka imekuwa vijana wengi wameathirika na kuishi katika hali ya wasiwasi. Akawa hajui ajinasibishe na kikundi gani. Sasa hapa tukatoa jawabu kutokamana na Aya na hadeeth mbili zilizotangulia. Fuata njia ya Waumini! Njia ya Waumini hawa wa zama hizi zetu? Jawabu ni La, tunamaanisha Waumini waliotutangulia wa zamani - enzi za mwanzo - enzi za Maswahaba - Salaf As-Saalih (watu wema waliotutangulia). Hawa ndiwo watu ambao inatupasa sisi kuwachukulia kuwa ndiwo mfano kwetu na watu ambao tufaao kuwaiga. Na wala hakuna mtu yoyote aliye sawa na wao katika uso wa Ulimwengu. Kwahivyo, kiini haswa cha ulinganizi wetu umestawi juu ya nguzo tatu - juu ya (1) Qur'aan, (2)

Sunnah na (3) Kuwaandama Salaf As-Saalih (watu wema waliotutangulia). Kwahivyo yoyote anaedai yakwamba anafuata Qur'aan na Sunnah, na kwamba hawafuati Salaf As-Saalih, na akawa amejimakini kwa maneno na vitendo: "Wao ni watu kama ambavyo sisi ni watu" [Yaani: wao na Maswahaba ni sawa au daraja moja], basi mtu huyu atakuwa amepotea upotofu ulio mbali. Kwanini? - Kwa sababu hakukubaliana na maneno tuliyowatajia sasa hivi. Je, aliifuata **"Njia ya Waumini"?** La. Aliwaandama Maswahaba wa Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam)? La. Ni kipi alichokifuata? Alifuata matamaniwa yake na akaifuata akili yake. Kwani akili ya mtu imeepukana na makosa na kuwa huru na madhambi? Jawabu ni La. Hivyo-basi, atakuwa katika upotofu ulio dhahiri. Mimi naamini yakwamba sababu ya ikhtilafu nyingi zilizorithiwa katika vipote mashuhuri vya zamani na kutafautiana kulikozuka katika siku za hivi karibuni ni kwa ukosefu wa kurudi kwenye hii asili ya tatu, ambayo ni Salaf As-Saalih.

Kila mmoja anadai yakwamba anafuata Qur'aan na Sunnah, na ni mara ngapi ambapo tushawahi kuyasikia maneno kama hayo kutoka kwa vijana waliochanganyikiwa, wanaposema: "Yaa Akhee, hawa jamaa wanadai yakwamba wanaifuata Qur'aan na Sunnah, na wale nao pia wanadai kuifuata Qur'aan na Sunnah". Sasa ukweli uko wapi baina ya hawa wawili? Ni Qur'aan na Sunnah na mfumo wa Salaf As-Saalih. Yeyote anaefuata Qur'aan na Sunnah bila ya kuwaandama Salaf As-Saalih, yeye kwa hakika atakuwa hajaifuata Qur'aan na Sunnah, bali atakuwa ameifuata akili yake tu, kama si hawaa (mapendelewa) ya nafsi yake.

Nitawapa mifano katika kuwafafanulia mas-ala haya - zaidi hii nukta iliyo muhimu, ambayo ni (kuuandama) mfumo wa Salaf As-Saalih. Kuna maneno yaliyonukuliwa kutoka kwa Al-Faarooq, 'Umar Ibn al-Khattaab (Radhiallaahu 'anhu) ambamo alisema: "Ikiwa watu wazushi na wenye kufuata hawaa' watajadiliana na wewe kwa kuitumia Qur'aan, basi nawe jadiliana nao kwa kutumia Sunnah..."

Ni kitu gani kilichomfanya 'Umar (Radhiallaahu 'anhu) kuyasema maneno kama hayo? Ni kutokamana na maneno ya Allaah pindi Alipokuwa Akizungumza na Mtume

Muhammad (Sallallaahu 'alayhi wasallam) (kama ilivyofasiriwa:

وَأَنزَلْنَآ إِلَيْكَ ٱلذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ

"Na tumekuteremshia *dhikr* (ukumbusho, Sunnah) ili (Ewe Muhammad) Uwabainishie watu yaliyoteremshwa kwao." [Soorah An-Nahl 16:44]

Jee, inawezekana kwa Muislamu, ambae ni bingwa wa lugha ya kiarabu, mwenye ujuzi wa hukmu na sarufi zake, kuweza kuifahamu Qur'aan bila ya kuitumia njia ya Mtume wetu (Sallallaahu 'alayhi wasallam)? Jawabu ni Laa! Basi iwapo jambo hilo haliwezekani, ndio maneno ya Allaah (kama yalivyofasiriwa): **ili (Ewe Muhammad) Uwabainishie watu yaliyoteremshwa kwao."**, hayangelikuwa na maana yoyote. Na maneno ya Allaah ni yenye kuepukana na sifa hiyo ya kutokuwa na maana yoyote. Kwahivyo, mtu yoyote mwenye kutafuta njia ya kuifahamu Qur'aan kwa kupitia njia isiyokuwa ya Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam), basi huyo amepotea vibaya sana.

Juu ya hayo, unadhania mtu huyo-huyo (alietajwa hapo juu) ataweza kuifahamu Qur'aan na Sunnah kwa kupitia njia nyengine yoyote isiyokuwa njia ya Maswahaba na Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam). Jawabu vile-vile itakuwa ni Laa! Na hii ni kutokamana na uhakika yakwamba wao (Maswahaba) ndiwo waliotupasha sisi riwaya zote, kwanza maneno (yanayosemwa) ya Qur'aan, ambayo Allaah Aliyoyateremsha katika moyo wa Muhammad (Sallallaahu 'alayhi wasallam). Na pili, wao ndiwo waliotupasha riwaya zenye ufafanuzi (wake), ambao uliotajwa kwenye Aya iliyotangulia, na vile-vile ufafanuzi wake (kwa njia ya vitendo) wa hii Qur'aan Tukufu.

Ufafanuzi wa Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam) wa Qur'aan unaweza kuwa na vigawanyo vitatu: 1) Maneno 2) Vitendo na 3) (kuwa kimya) Kuruhusu. Ni kina nani waliotuhadithia kuhusu maneno ya Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam)(?) - Maswahaba zake. Ni kina nani waliotuhadithia kuhusu vitendo vya Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam)(?) - Maswahaba zake. Ni kina nani waliotuhadithia kuhusu kulinyamazia jambo kwa njia ya kuliruhusu(?) - Maswahaba zake. Basi kwa ajili hii, ni

jambo lisilowezekana kwetu sisi kutegemea ubingwa wetu wa lugha peke yake katika kuifahamu Qur'aan. Bali inatulazimu kutafuta msaada katika kuifahamu Qur'aan. Lakini hiyo haimaanishi yakwamba hatuihitaji lugha (ya kiarabu) kabisa kwenye mas-ala haya, Laa!

Hiyo ndiyo sababu sisi tunaitaqidi yakwamba waajemi (wale ambao lugha ya kiarabu kwao ni ya kigeni), ambao wasoijua lugha ya kiarabu vile inavyostahiki, huingia kwenye makosa mengi mno. Na huzidi kuzama kwenye makosa, kwani wao huteleza kwenye huu msingi mbovu wa kutoregea kwa wale Salaf As-Saalih katika kuifahamu Qur'aan na Sunnah. Mimi simaanishi kwa maneno niliyoyasema hapo awali yakwamba hatuwezi kuitegemea lugha (ya kiarabu) katika kuifafanua Qur'aan. Itakuwaje hivyo? - kwani tukitaka kuyafahamu maneno ya waarabu basi hapana shaka - ni lazima tuifahamu lugha ya kiarabu. Vile-vile, maadamu mtu atataka kuifahamu Qur'aan na Sunnah, itampasa aijue lugha ya kiarabu.

Kwahivyo sisi tunasema, **Ufafanuzi** huwo wa Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam), uliotajwa katika Aya hiyo iliyotangulia, umegawanywa kwenye mafungu matatu: Maneno yake, vitendo vyake na kuruhusu jambo kwa njia ya kulinyamazia. Tutawapa mfano katika kuwafahamisha yakwamba vigawanyo hivyo ni jambo lililothubutu, lisilokuwa na pingamizi yoyote. Amesema Allaah ('azza wa jall)(kama ilivyofasiriwa:

وَٱلسَّـارِقُ وَٱلسَّـارِقَةُ فَـٱقْطَعُوٓاْ أَيْدِيَهُمَـا

"Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, ikateni mikono yao." [Soorah al-Maa'idah 5:38]

Hebu angalia jinsi ambavyo isivyowezekana kwetu sisi kuifahamu Qur'aan kulingana na lugha peke yake. Mwivi, kulingana na lugha ni mtu yoyote anae-iba kitu kutoka katika sehemu fulani iliyo chini ya hifadhi, pasi na kujali iwapo kitu hicho kina thamani au la. Kwa mfano mtu ameiba yai au mkate wa bofulo - Huyu kulingana na lugha (ya kiarabu) anachukuliwa kuwa ni mwivi. Amesema Allaah (azza wajall'):**"Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, ikateni mikono yao."**Jee, kila anaeiba atawajibika kukatwa

mkono? Jawabu ni la. Kwanini? Ni kwa sababu yule mwenye kutufafanulia (yaani: Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam)), ambae ni juu yake kulifafanua lile jambo linaloelezwa (yaani: Qur'aan) ametueleza wale wanaostahiki kukatwa mikono miongoni mwa wevi. Mwenye kutufafanulia ni Mtume na kinachofafanuliwa ni Qur'aan. Akasema Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam): **"Musiukate mkono isipokuwa kwa (mwenye kuiba) robo ya dinaar na ziada ya hapo."** Kwahivyo kila anaeiba kitu chenye thamani isiyotimia robo ya dinaar, hata kama kulingana na lugha, mtu huyo anaitwa mwivi, hadhaniwi kuwa ni mwivi kulingana na maelezo ya kisheria.

Sasa hapa, tunakuja kwenye uhakika wa ki-ilimu, ambao wanafunzi wengi wa ki-ilimu hawaujui. Kwa upande mmoja tuna lugha ya kiarabu, iliyohifadhiwa na vizazi vya kila zama. Na kwa upande mwengine tuna lugha ya kisheria; ambayo Allaah (azza wajall') ndie Aliyeipa jina hilo na kuieleza, ambayo Waarabu - waliokuwa wakiizungumza lugha hiyo ya Qur'aan (yaani: Kiarabu), ambayo ndiyo lugha iliyoteremshiwa Qur'aan - hawakuwa wakiijua kabla ya hapo. Kwahivyo ikiwa mwivi itachukuliwa, kulingana na lugha ya kiarabu, basi itawahusu wevi wote. Lakini iwapo mwivi atachukuliwa kulingana na ufahamu wa kisheria, basi hawatohusika wevi wote, lakini watakaohusika watakuwa ni wale wenye kuiba kilicho sawa na robo ya dinaar au zaidi ya robo ya dinaar. Basi huwo ni mfano wa kweli - Sisi hatuwezi kuitegemea ilimu yetu ya lugha ya kiarabu peke yake katika kuifahamu Qur'aan na Sunnah. Haya ni makosa ambayo waandishi wengi wa zama hizi wameteleza. Huitanguliza ilimu yao ya lugha ya kiarabu kabla ya Aya za Qur'aan na hadeeth za Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam). Kwahivyo wao huyafasiri maneno ya kisheria mara wakaja na tafsiri za uzushi, ambazo Waislamu hawajawahi kuzisikia hapo awali.

Kutokana na hayo sisi twasema, ni wajibu kufahamu yakwamba mwito wa kweli wa Uislamu umejengwa juu ya Asili 3 za kimsingi, ambazo ni: 1) Qur'aan; 2) Sunnah; na 3) Njia na jinsi walivyofahamu Salaf As-Saalih. Kwahivyo, ni makosa kuifasiri Aya isemayo **"Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke** kulingana na mahitaji ya ki-lugha. Ni sharti ilingane na mahitaji ya lugha ya kisheria; isemayo: **"Musiukate mkono isipokuwa kwa (mwenye kuiba) robo ya dinaar na ziada ya hapo."**

Sehemu iliyobaki ya Aya yasema (kama ilivyofasiriwa): **"Ikateni mikono yao."** Ni upi mkono katika desturi ya ki-lugha? Wote huu huitwa mkono - kuanzia kwenye ncha za vidole hadi kwenye makwapa - wote huu ni mkono. Sasa jee, huu mkono unatakikaniwa ukatwe kutoka hapa, au hapa, au hapa? Rasoolullaah (Sallallahu 'alayhi wasallam) ametufafanulia hayo yote kwa vitendo vyake [yakwamba inatakikaniwa kukatwa kwenye kiungo cha kiganja]. Hakuna hadeeth iliyo saheeh - kama ile iliyothibitisha mwivi anaepasa kukatwa mkono wake - hatuna hadeeth inayoeleza waziwazi mahali pa mkono itakikaniwapo kukatwa, kutoka katika **Ufafanuzi** wa maneno ya Mtume (Sallallahu 'alayhi wasallam). Badala yake paliteremshwa **Ufafanuzi** wake wa vitendo - jinsi alivyotekeleza kwa vitendo. Na tulijuaje kuhusu kitendo hicho chake(?) Kutoka kwa Salaf As-Saalih - maswahaba wa Mtume (Sallallahu 'alayhi wasallam). Hicho ni kiwango cha pili, ambacho ni **Ufafanuzi** wa vitendo. Kiwango cha tatu ni jinsi Mtume (Sallallahu 'alayhi wasallam) alivyoruhusu jambo lolote lifanywe; na asilipinge wa kulikataza. Na kuruhusu huko si kwa njia ya maneno kutoka kwake wala kitendo kutoka kwake; bali ni kitendo kilichotendwa na mtu mwengine, ambacho yeye Mtume (Sallallahu 'alayhi wasallam) alichokishuhudia na akakiunga mkono. Kwahivyo iwapo Mtume (Sallallahu 'alayhi wasallam) ameona jambo fulani na akalinyamazia, na kukiruhusu kinakuwa ni kitu kinachoruhusiwa na kufaa, lakini kama aliona jambo fulani na akalipinga, hata kama jambo hilo limefanywa na baadhi ya Maswahaba zake, hata kama limeswihi kutoka kwake yakwamba alilikataza, basi inakuwa makatazo hayo yatakuwa na nguvu juu ya yale aliyoyaruhusu. Wacha niwape mfano wa haya mambo mawili kulingana na Ahaadeeth.

Amesema 'Abdullaah Ibn 'Umar Ibn Al-Khattaab (Radhiallaahu 'anhu): **"Tulikuwa tukinywa haliyakuwa tumesimama na tulikuwa tukila haliyakuwa tunatembea katika wakati wa uhai wa Mtume (Sallallahu 'alayhi wasallam)."**

Sasa kwenye hadeeth hii, 'Abdullaah ametupasha habari kuhusu mambo mawili: 1)Kunywa haliyakuwa umesimama, na 2) Kula haliyakuwa unatembea.

Na akasema yakwamba mambo hayo mawili yalifanywa katika wakati wa Mtume (Sallallahu 'alayhi wasallam). Sasa ni nini hukmu ya kisheria kuhusu mas-ala haya mawili: Kunywa haliyakuwa umesimama na kula haliyakuwa unatembea?

Tukitumia vipimo tulivyovitaja hapo awali, tutaweza kuifikia hukmu - bila ya shaka - pamoja na mahitaji ya ziada, ambayo ni mtu awe anajua mambo ambayo Mtume (Sallallahu 'alayhi wasallam) aliyoyakataza, kwa njia ya kutamka, kitendo na (kimya cha) kuruhusu.

Tukilipima suala hili katika Sunnah saheeh, kuhusu jambo la kwanza (kunywa haliyakuwa umesimama), ambalo idadi kubwa ya Waislamu, kama si wengi wao, wako katika mtihani leo. Na huko (kunywa haliyakuwa umesimama) ni kwenda kinyume na maneno ya Mtume (Sallallahu 'alayhi wasallam). Wanakunywa haliyakuwa wamesimama, wao (yaani: wanaume) wanavaa dhahabu na hariri. Huu ni ukweli usiofichika. Lakini jee, kwani Mtume (Sallallahu 'alayhi wasallam) aliyakubali yote hayo? Jawabu ni kwamba aliyaruhusu na kuyakataza baadhi fulani ya mambo. Kwahivyo kila alichokikataza kinaangukia katika mipaka ya maovu (Munkar) na kila alichokiruhusu kinaangukia katika mipaka ya uzuri (Ma'roof). Sasa amekataza kunywa haliyakuwa umesimama katika ahaadeeth chungu nzima. Na wala mimi sitaki kuanza kuzitaja ahaadeeth zote - ili kwanza tusizumbue mengine kutoka katika wakati ambao tuliojipinda nao kuhusu kulijadili suala hili ili tuweze kuchukua masuali tutakapomaliza, na pili, suala hili linahitaji kikao chake mahsusi.

Lakini inatosheleza kuleta hadeeth moja iliyo saheeh, iliyopokelewa na Imaam Muslim kutoka katika Saheeh yake, kutoka katika riwaya ya Swahaba Anas Ibn Maalik (Radhiallaahu 'anhu) aliyesema:

"Rasoolullaah (Sallallahu 'alayhi wasallam) alikataza kunywa haliyakuwa umesimama."

Na katika riwaya nyengine (ya hadeeth), alisema: **"Rasoolullaah (Sallallahu 'alayhi**

wasallam) aliwazuia (wengine) wasinywe haliyakuwa wamesimama."

Kwahivyo, jambo hili lililokuwa likifanyika wakati wa uhai wa Mtume (Sallallahu 'alayhi wasallam), kama ilivyoshuhudiliwa kwenye riwaya ya Ibn 'Umar (Radhiallaahu 'anhu), liliachwa na kuzuiwa. Kwahivyo jambo walilokuwa wakifanya likakatazwa kutokana na makatazo ya Mtume (Sallallahu 'alayhi wasallam) kuhusiana nalo. Lakini kwenye sehemu ya pili ya hadeeth (ya Ibn 'Umar) isemayo yakwamba walikuwa wakila haliyakuwa wakitembea, hawakupata habari zozote yakuwa Mtume (Sallallahu 'alayhi wasallam) amelikataza jambo hilo. Kutokana na (kimya hicho cha) kuruhusu, kunapata hukmu ya ki-dini. Mpaka hapa tulipofika, tumekuja kujua jinsi ya umuhimu wa kutegemea njia ya Salaf As-Saalih katika kuifahamu Qur'aan na Sunnah. Na pia, yakwamba hapana yoyote awezae kuitegemea ilimu yake, kama si makosa kusema ujinga wake, katika kuifahamu Qur'aan na Sunnah.

Baada ya kuibainisha hali hii iliyo muhimu ya **juu ya njia (mfumo) ya Salaf As-Saalih",** imenilazimu niwape mifano. Zamani Waislamu walitawanyika katika vipote vingi sana, ushawasikia Mu'tazilah, ushawasikia Murji'ah, ushawasikia Khawaarij, ushawasikia Zaydiyyah, pasi na kuwasahau Shi'ah na ma-Raafidhah. Hapana yoyote miongoni mwa haya mapote, licha ya upotofu mkubwa walio nao, asiejishirikisha na maneno hayo yasemwayo na Waislamu, ambayo ni: "Sisi tupo juu ya Qur'aan na Sunnah." Hapana yoyote miongoni mwao asemae: "Sisi hatufuati Qur'aan na Sunnah." Na lau mmoja wao atasema hivyo, atakuwa ameuacha mviringo wa Uislamu. Sasa ni kwanini wamegawanyika ikiwa wote wao wameitegemea Qur'aan na Sunnah - na mimi nashuhudia yakwamba hawaitegemei Qur'aan na Sunnah kwa msaada wowote. Kwani kuitegemea huku (hufanywa vipi) huwaje? Huwa inafanywa bila ya kujitegemeza na msingi wa tatu, ambao ndio ule waliosimama nao Salaf As-Saalih.

Na pana nukta ya ziada hapa ambayo inatulazimu kuijua - nayo ni kwamba Sunnah ni tafauti kabisa na Qur'aan Tukufu kwa maana yakwamba Qur'aan Tukufu ni ile iliyohifadhiwa baina ya magamba mawili ya mus-haf, kama ijulikanavyo na kila mmoja. Lakini kuhusu Sunnah, basi sehemu yake kubwa, imetapakaa kwa mamia, kama sio

maelfu ya vitabu ambavyo miongoni mwake, kuna idadi kubwa yake ingali kwenye ulimwengu wa maficho - Ulimwengu wa maandishi ya mikono ambayo hayajachapishwa.

Zaidi ya hayo, hata hivi vitabu ambavyo baadhi yake viko kwenye uchapishwaji leo, kuna vile vyenye ahaadeeth Saheeh na vile vyenye ahaadeeth dha'eef. Sasa wale wanaotegemea Sunnah kwa usaidizi, iwapo wao ni miongoni mwa Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah na mfumo wa Salaf As-Saalih au wao wanatokamana na vikundi vyengine - wengi wao hawawezi kutafautisha baina ya Sunnah Saheeh na Sunnah dha'eef. Kwahivyo mwishoe wao hupotea na kuanza kuhitilafiana na kwenda kinyume na Qur'aan na Sunnah kwa ajili ya kujitegemeza kwao na ahaadeeth dha'eef na maudhoo'. Jambo ninalosisitiza hapa ni kwamba baadhi ya vikundi hivi ambavyo tulivyovitaja hapo juu hupinga maana za dhahiri zilizotajwa kwenye Qur'aan na Hadeeth Saheeh, katika nyakati za zamani na hata katika nyakati hizi zetu. [Kwa mfano] Qur'aan Tukufu imetueleza na kutoa bishara kwa Waumini kuhusu neema kubwa sana watakayoipata wakiwa peponi, ambayo ni Mola wa Ulimwengu Atajitokeza kwao kwa Nafsi Yake nao watamuona. Kama alivyosema mwanachuoni mmoja wa ki-Salafee:

"Waumini watamuona Yeye, (sisi twaamini hayo) bila ya kusema itakuwaje au kujaribu kulinganisha, au kutoa mifano yake (ya jinsi itakavyokuwa)."

Maandishi ya ushahidi kutoka katika Qur'aan na Sunnah yanathibitisha. Sasa itakuwaje baadhi ya vipote hivi vya zamani na vya sasa wanaipinga neema hii? Ama kuhusu vile vikundi vya zamani vilivyopinga huko kumuona (Allaah), basi palikuwepo na Mu'tazilah. Leo, kulingana na nijuavyo mimi, hapana kikundi chochote katika uso wa Ulimwengu kisemacho: "Sisi ndio Mu'tazilah. Tunaandama mafundisho ya Mu'tazilah." Hatahivyo, nilimuona mtu mmoja mpumbavu aliyejitangaza waziwazi yakwamba yeye ni Mu'tazilee. Na anakanusha mambo mengi ya kweli yaliyo-thibitishwa katika dini, kwa sababu yeye alikuwa ni mtu wa kujivurumiza. Sasa hawa Mu'tazilah wameipinga hii neema kubwa na wakasema kwa kutumia fahamu zao dhaifu: "Ni jambo lisilowezekana yakwamba Allaah Anaweza kuonekana!" Kisha wakafanyaje? Jee, waliikataa Qur'aan? Akasema Allaah (azza wajall) (kama ilivyofasiriwa):

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاضِرَةٌ ﴿٢٢﴾ إِلَىٰ رَبِّهَا نَاظِرَةٌ ﴿٢٣﴾

"Nyuso (nyengine) siku hiyo zitang'ara (kweli kweli). Zinamtazama Mola wao." [Soorah al-Qiyaamah 75:22-23]

Jee, waliikataa Aya hii? Laa hawakuikataa, hawakukufuru, wala hawakuikanusha dini. Mpaka hivi leo, Ahlus-Sunnah wa kikweli wameipasisha yakwamba hawa Mu'tazilah wako juu ya upotofu lakini hawawatoi kwenye mviringo wa Uislamu. Na sababu ni kwamba wao hawaipingi Aya hii, lakini ukweli ni kwamba wamekataa maana yake haswa iliyokusudiwa, ambayo **Ufafanuzi** wake umeelezwa katika Sunnah, ikiwa twakumbuka. Amesema Allaah (Subhaanahu wata'aalah) kuhusu Waumini watakaoingia peponi (kama ilivyofasiriwa): **"Nyuso (nyengine) siku hiyo zitang'ara (kweli kweli). Zinamtazama Mola wao."** Kwahivyo wakabadilisha maana yake - wameamini maneno (matamshi) ya Aya hiyo, lakini hawakuamini maana yake. Na matamshi yenyewe, kama walivyosema wanavyuoni ndiyo makusudiwa ya maana. Kwahivyo, tunapoyaamini matamshi lakini tusiiamini maana yake, basi (Imani hii) **Huwa haizidishi wala haipunguzi njaa.** [haifaidishi chochote]

Basi ni kwanini watu hawa kukanusha huko kumuona Allaah? Fahamu zao zimebanwa na kuzuiwa wasije wakadhania na kuanza kuwaza yakuwa mja huyu ('abd), aliyeumbwa na aliye na sifa za upungufu ana uwezo wa kumuona Allaah wazi wazi. Ni kama vile Mayahudi walivyomtaka Musa (ili wamuone Allaah), basi Allaah Akawakatalia kama ilivyo katika kisa mashuhuri [Tizama Soorah al-Baqarah 2:55-59]; Allaah Akamwambia Musa (kama ilivyofasiriwa):

قَالَ لَن تَرَىٰنِي وَلَٰكِنِ انظُرْ إِلَى الْجَبَلِ فَإِنِ اسْتَقَرَّ مَكَانَهُ فَسَوْفَ تَرَىٰنِي

"Akasema (Allaah): Hutaniona, lakini tazama jabali (lililoko mbele yako). Kama litakaa mahali pake (bila kupasuka na kutawanyika) utaweza kuniona." [Soorah al-

A'raaf 7:143]

Akili zao zilichongeka kiasi cha kwamba wakajihisi yakuwa wamewajibika kuichezea Qur'aan na wakawa tayari kubadilisha maana yake. Kwanini (?) - kwa sababu Imani zao kuhusu mambo ya kufichamana ni dhaifu na Imani zao kuhusu akili zao ina nguvu kuliko Imani yao katika mambo ya kufichamana , ambayo ndiyo waliyoamrishwa washikamane nayo, katika mwanzo wa Soorat al-Baqarah:

الٓمٓ ﴿١﴾ ذَٰلِكَ ٱلۡكِتَٰبُ لَا رَيۡبَۛ فِيهِۛ هُدٗى لِّلۡمُتَّقِينَ ﴿٢﴾ ٱلَّذِينَ يُؤۡمِنُونَ بِٱلۡغَيۡبِ

"Alif Lam Mym. Hiki ni Kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake; ni uwongozi kwa Muttaqeen (wamchao Allaah) - (ni kina nani hao?). Ambao huyaamini yasiyoonekana." [Soorah al-Baqarah 2:1-2]

Ni miongoni mwa sifa za Allaah yakuwa Yeye Haonekani, kwahivyo kila wakati Allaah (azza wa jall') anapojisifu, hatuna budi tujue huwo ni ukweli na tuukubali kwa sababu akili zetu ni pungufu. Mu'tazilah hawakuipasisha nukta hii, na hiyo ndiyo sababu walikataa na kupinga ukweli mwingi uliothubutu kwenye dini kama maneno ya Allaah yasemayo (kama yalivyofasiriwa): **"Nyuso (nyengine) siku hiyo zitang'ara (kweli kweli). Zinamtazama Mola wao."**

Vile vile katika Aya nyengine iliyofichamana zaidi kwa watu hawa kuliko Aya ya mwanzo; nayo ni maneno Yake Allaah yasemayo (kama yalivyofasiriwa):

لِّلَّذِينَ أَحۡسَنُواْ ٱلۡحُسۡنَىٰ وَزِيَادَةٞۖ

"Wale waliofanya wema watapata *Al-Husnaa* na *Ziyaadah* (nyongeza juu ya hayo)." [Soorah Yoonus 10:26]

Al-Husnaa (wema) hapa maana yake ni pepo na ***Ziyaadah*** (kuzidi) hapa maana yake ni, kumuona Allaah siku ya Qiyaamah. Haya ndiyo yaliyosemwa katika hadeeth

iliyopokelewa katika Saheeh Muslim na upokezi Saheeh wa riwaya kutoka kwa Sa'd Ibn Abee Waqqaas (Radhiallaahu 'anhu) aliyesema: Amesema Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam): **"Kwa wale watu wafanyao wema, watalipwa *Al-Husnaa*- (maana yake) Pepo - na *Ziyaadah* - (maana yake) kumuona Allaah."**

Hawa Mu'tazilah na Ma-Shi'ah, ambao ni Mu'tazilah kulingana na kanuni za Imani zao, wanapinga kuhusu kuonekana kwa Allaah, jambo ambalo lililothubutu katika Aya ya kwanza na kufafanuliwa na Rasoolullaah (Sallallaahu 'alayhi wasallam) katika Aya ya pili. Na kuna Ahaadeeth nyingi (zinazofika daraja ya Mutawaatir) kutoka kwa Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam) kuhusiana na suala hilo. Kwahivyo, Ta'weel yao hiyo (ya kupotoa maana ya kihakika) ya Qur'aan kumewafanya wazipinge Ahadeeth zilizo Saheeh za Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam). Wakawa wamejiondoa kutoka katika ubora wa kudhaniwa kuwa kikundi kitakacho okoka - **"Yale tuliyojiambatanisha (nayo) mimi na Maswahaba zangu."** Rasoolullaah (Sallallaahu 'alayhi wasallam) aliamini na akawa na Imani thabiti yakwamba Waumini watamuona Mola wao, kwa sababu ilipokelewa kwenye Saheeh mbili kutoka katika riwaya za kikundi kikubwa cha Maswahaba, kwa mfano Abu Sa'eed Al-Khudhree, Anas Ibn Maalik - na mbali na vitabu vya Saheeh - alikuwepo Abu Bakr As-Siddeeq na kadhaalika. Akasema Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam):

"Kwa hakika mutamuona Mola wenu siku ya Malipo, kama vile muuonavyo mwezi katika usiku (ung'arao) wenye mwezi mpevu - hamuna matatizo yoyote katika kuuona."

Maana inayokusudiwa hapa, ni kwamba hamutokuwa na matatizo yoyote katika kumuona Allaah kama vile pasipokuwa na matatizo yoyote katika kuuona mwezi kwenye usiku ung'arao pakawa na mwezi mkubwa, bila ya kutanda mawingu. Walizikataa ahaadeeth hizi kulingana na akili zao, kwahivyo wakawa ni dhaifu wa Imani.

Huu ni mfano mmoja wa mambo ambayo baadhi ya vipote vya zamani vilianguka na kutumbukia humo, na pia baadhi ya vipote vya siku hizi, kama vile Ma-Khawaarij,

wanaoamini hivyo pia. Vilevile kwenye orodha hiyo, wanapatikana Ma-l'badhi (Ibaadiyyah) ambao nao siku hizi wamekuwa washupavu kwenye kuwalingania watu katika upotofu wao. Wamekuwa na nakala na vitabu vidogo wanavyovisambaza na kupeana, na kufufua mambo mengi ya upotofu, (ambayo Ma-Khawaarij waliyotambulika nayo) katika siku zilizopita, kama vile wanavyokanusha yakuwa Allaah (Subhaanahu wata'aalah) ataonekana Peponi.

Sasa tutawaletea mfano tulonao leo, ambao ni Ma-Qadiyani. Pengine ushawahi kuwasikia. Hawa jamaa husema kama tusemavyo sisi: "Nashuhudia yakwamba hapana mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah, na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah." Wanaswali swala tano kila siku, wanasimamisha swala ya ijumaa, wanafanya Hajj na 'Umra katika nyumba Tukufu ya Allaah. Hakuna tafauti baina yetu sisi na wao wao ni kama Waislamu. Hatahivyo, wanatafautiana na sisi katika mas-ala ya misingi ya Imani na kanuni zake, kama vile imani zao yakwamba Utume haukumalizika. Wanaamini yakwamba Mitume watakuja baada ya Muhammad na wanadai yakwamba tayari mmoja wao ashakuja kwa Qadiyani, mji fulani ulioko India. Kwahivyo (wanasema yakwamba) yeyote ambae asiyemuamini Mtume huyo aliyewajilia wao basi atakuwa Kafiri. Watasemaje hivyo, ikiwa Aya ipo waziwazi (kama ilivyofasiriwa):

مَّا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَآ أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ وَلَـٰكِن رَّسُولَ ٱللَّهِ وَخَاتَمَ ٱلنَّبِيِّـۧنَ

"Muhammad si baba wa yoyote katika wanaume wenu, bali yeye ni Mtume wa Allaah na mwisho wa Mitume" [Soorah Al-Ahzaab 33:40]
Wataletaje madai hayo, ikiwa ahaadeeth zimefikia kiwango cha Tawaatur (zikisema): "Hapana Mtume mwengine baada yangu." Kwahivyo wakabadilisha maana ya Qur'aan na Sunnah na hawakuzifasiri Qur'aan na Sunnah kama vile walivyozifasiri Salaf As-Saalih. Na Waislamu nao pia wakawaandama kwa hayo bila ya kuwa na pingamizi yoyote baina yao, mpaka alipokuja huyu mpotofu aliye kwenye njia ya upotevu, aitwae Mirza Ghulaam Ahmad Al-Qadiyaanee aliyedai Utume. Na ana kisa kirefu mtu huyu, lakini sasa hivi hilo si lengo la somo letu. Basi akawalaghai watu wengi ambao wasiokuwa na ilimu ya ukweli wa mambo haya, yenye kumuhifadhi Muislamu asipotoke

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

kama walivyopotoka na huyu Dajjaal aliyejidai Utume yeye mwenyewe.

Walifanyaje na maneno ya Allaah (Subhaanahu wata'aalah) yasemayo (kama ilivyo katika tafsiri): **"Bali yeye ni Mtume wa Allaah na mwisho wa Mitume?"** Wanasema hiyo haimaanishi yakwamba hakuna Mtume baada yake, lakini neno *Khaatam* lina maana ya pambo la Mtume. Kwahivyo, kama vile *Khaatam* (muhuri au pete) ni pambo la kidole, basi vile vile, Muhammad ni pambo la Mitume. Nao pia hawakuikataa aya. Hawakusema yakwamba Allaah hakuiteremsha Aya hii kwenye moyo wa Muhammad. Bali wamekufuru katika maana yake haswa iliyokusudiwa. Sasa pana uzuri gani katika kuyaamini maneno ikiwa huamini maana iliyokusudiwa ya maneno hayo. Ikiwa huna shaka kuhusu ukweli huu, basi ni njia ipi ambayo itakayokuleta kwenye kufahamu maana ya Qur'aan na Sunnah. Tayari ushaijua njia. Si juu yetu kuitegemea ilimu yetu ya lugha ya kiarabu, wala kuifasiri Qur'aan na Sunnah kwa matamanio yetu au kwa mila zetu, au kuandama madh-hab zetu ki-Upofu au amri zetu za Ki-Soofee, lakini njia ya kipekee ni - kama isemwavyo kwa kawaida na nitayamalizia maneno yangu kwa haya:

"Na kila zuri ni katika kufuata wale waliotutangulia (Salaf),
Na kila Ovu ni katika uzushi wa wale waliokuja baadae (Khalaf)."

Tunatarajia yakwamba hii itatosheleza kama,

إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَذِكْرَىٰ لِمَن كَانَ لَهُۥ قَلْبٌ أَوْ أَلْقَى ٱلسَّمْعَ وَهُوَ شَهِيدٌ ﴿٣٧﴾

"Ukumbusho kwa mwenye moyo au kwa ategaye sikio, naye mwenyewe awe hadhiri." [Soorah Qaaf 50:37].